



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA TARIME**  
*(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi)*



**Simu Na.: +255 28 2690218**  
**Nukushi: +255 28 2690218**  
Barua pepe: [ded@tarimedc.go.tz](mailto:ded@tarimedc.go.tz)  
Tovuti: [www.tarimedc.go.tz](http://www.tarimedc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri wilaya  
S.L.P 16,  
**TARIME**

**UnapojibuTafadhaliTaja:**  
Kumb Na. HWT/L1/54

22 agosti, 2022

## **TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Tarime anapenda kuwataarifu wote walioomba kazi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III na Katibu Mahsusi III, nafasi iliyotanganzwa kupitia tangazo Kumb. Na. HWT/L1/53 la tarehe **23 Mei, 2022** kuwa usaili unatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **30/08/2022** hadi tarehe **03/09/2022** kama jedwali ilivyoainisha hapo chini.

Waombaji ambao majina yao hayajaonekana kwenye orodha iliyoambatishwa pamoja na tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo hitajika.

Aidha watakaofaulu mtihani wa mchujo majina yao yatawekwa katika TOVUTI ya Halmashauri ya wilaya Tarime ([www.tarimedc.go.tz](http://www.tarimedc.go.tz)) na yatabandikwa kwenye mbao za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

**Wasailiwa walioitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-**

- Wasailiwa wote waje na vyeti vyao halisi ( original) siku ya usaili. Cheti cha kidato cha nne (form four) , cheti cha Astashahada ( Certificate au Technician NTA Level 5).
- Kwa makatibu mahsusi daraja la III aje na cheti cha uhazili chenye ufaulu wa mtihani hatua ya tatu, cheti cha kompyuta katika program za windows, microsoft office, internet, E-mail na publisher.

- Kila msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi, vitambulisho vinavyo mtambulisha ni pamoja na, kitambulisho cha mkazi, kitambulisho cha uraia (NIDA), kitambulisho cha mpiga kura au hati ya kusafiria (passport) na leseni ya Udereva.
- Msailiwa ambaye hata fika na nyaraka zilizoainishwa hapo juu hataruhusiwa kufanya usaili.
- Kila msailiwa atajigharamia kwa Chakula, Malazi na Usafiri.
- **Testimonials “Provisional Results” “Statements of results” Hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita (Form IV na Form VI) HAVITAKUBALIKA.**

Pia mnashauriwa kutembelea tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ([www.tarimedc.go.tz](http://www.tarimedc.go.tz)) ili kupata mabadiliko yoyote endapo yatajitokeza.

Usaili utafanyika katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Jakaya Kikwete (JK) Nyamwaga kuanzia **Saa 1:30 asubuhi**.

Aidha, ratiba ya usaili pamoja na majina ya waombaji waliokidhi vigezo kwa nafasi zilizo tangazwa limeambatanishwa chini ya tangazo hili.

Imetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.



Solomon I Shati  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**TARIME**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR  
TARIME DISTRICT COUNCIL



## RATIBA YA USAILI

NA	KADA	TAREHE YA USAILI YA MCHUJO	TAREHE YA USAILI WA VITENDO	TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO
1.	Katibu mahsusi	Hakuna	30/08/2022	31/08/2022
2.	Mtendaji wa mtaa/kijiji	01/09/2022	Hakuna	02/09/2022- 03/09/2022